Jiwe la Kujengea la Kiroho Na. 43

## AHADI YETU: KURUDISHIWA KWA ULE UUNGU.

***Katika Yoel 1:1-4 Na 2:23-27*** *Tunasoma habari za kuharibiwa kwa kanisa kla mungu na nyakati za kurudishiwa / kurejeshewa mambo yote. Na huu wakati umekuja sasa (Matendo 3:19-21)*

Kila muaminio aliyeunganishwa na mti. (Zaburi 1) lakini kanisa la wale walioteuliwa kimbele linaonyeshwa pia kama mti wa matunda wa Mungu. Ambao unapaswa kumzalia Mungu matunda ya aina tisa, matunda ya Roho ***(Wagalatia 5:22)***

Mti huu wa matunda ulikuwa umepandwa kutoka kwa Mungu. Siku ya Pentekoste, ukiwa una matunda yote tisa kwa uaminifu matunda ya Roho na karama zote tisa za Roho ***(1Kor 12:4-11)***

Tunasoma katika (***Matendo 2:42-47)***Na Mungu aliongeza kanisa kwa wale waliokuwa wakiokolewa. Hili liliendelea kwa muda gani. Sisi hatujui, lakini siku moja kama vile hawa alivyoshawishiwa na kudanganywa na shetani, Hivyo kanisa litachanganyika na roho ya mpinga kristo. "….Na hii ndio roho ya mpinga kristo ambayo mmesikia kwamba yaja na sasa imekwisha kuwako duniani ***(1Yohana 4:3)*** Na Yesu kuhusu Bibi harusi wake katika wakati ule wa kwanza alisema "Lakini nina neno juu yako yako ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza basi kumbuka ulipoanguka ukatubu" ***(Ufunuo 2:4-5)***[1]

Kwa hiyo katika wakati ule wa kwanza wa kanisa wa Efeso ambo ulikuwa tangu 53 – 170 AD tayari roho wa mpinga kristo ilikuwa imeshaanza. Ikiwakilishwa katika aina tofauti tofauti zapararazikitenda kwa uharibifu katika kanisa la Mungu.
Sasa nyuma kabisa kule lile kanisa la mwanzo( muda mfupi sana kabla ya Pentekoste) ule mzabibu wa uongo ukajifunganisha kuuzunguka ule mzabibu wa kweli na tunayona yale matendo ya wanikolai . Na hiyo roho itaonekana ikiwapiga vita ule mzabibu wa kweli mpaka itakapoharibiwa na Mungu.

Huu unikolai ni nini? Hili neneo linatokana na maneno mawili ya kigiriki. Nikao ikimaanisha kuwashinda, na Laosi inamaanisha washirika. Katika lugha ya wazi mtu fulani katika lile kanisa la kwanza alikuwa anajaribu kuwashinda washirika. Kama washirika walikuwa wanashindwa, hiyo ilikuwa ni mamlaka fulani iliyokuwa inafanya hivyo.
Ni kitu gani ambacho Mungu alikichukia ambacho kilikuwa kinatokea katika hilo kanisa? Ilikuwa ni kitu gani kilichokuwa kinaendelea hapo na kinaendelea hapo na kinaendelea leo, ni hasa kile nacho unikolai kilimaanisha. Watu walikuwa wanawekwa chini ya Mamlaka kwa namna ambayo ilikuwa kinyume kabisa na neno la Mungu. [2]

Sasa kwa nini hili ni jambo la kutisha? Ni la kutishakwa sababu Mungu kamwe hajaliweka kanisa lake mikononi mwa uongozi wa kuchaguliwa ambao unaenda na mawazo ya kisiasa. Ameliweka kanisa lake katika uangalizi wa watu waliowekwa na Mungu, waliojazwa na Roho, watu waongozao watu kwa kuwalisha neno. Hawajatenganisha watu katika makundi kwa namna ambayo washiriki wanaongozwa na ukuhani mtakatifu. Ni kweli kwamba inabidi uwe mtakatifu.Lakini kadhalika kusanyiko lote linapaswa kuwa hivyo. Zaidi ya hayo hakuna mahali katika neno ambapo mapadre au wahudumu au wowote wakifanya upatanisho kati ya Mungu na watu au mahali ambapo wametenganishwa katika ibada zao kwa bwana Mungu.

Mungu anataka wote wampende na kumtumikia pamoja. Unikolai unaharibu hizi kanuni na badala yake unatenganisha wahudumu na watu na kuwafanya viongozi kuwa mabwana badala ya watumishi

Kwa hiyo kile kilichoanza kama tendo katika wakati ule wa kwanza sasa limefanywa kuwa fundisho hasa. Na kadhalika ndivyo ilivyo leo. Maaskofu bado wanadai kuwa na nguvu za kutawala watu na wanatenda nao vile wapendavyo, kuwaweka pale ambapo wanapenda katika huduma. Hili linakataa uongozi wa Roho Mtakatifu. [3]
Na kama utaangalia kwa karibu hawa wadudu watatuwa ***Yoel 1:1-4*** ni mdudu yuleyule katika hatua tofauti, wa kwanza ni tunutu, halafu nzige, na halafu parare na madumadu. Tunaambiwa kuwa huyo ni mdudu yuleyule katika hatua tofauti akija chini. [4]
Kuja kwa kwanza

Yule tunutu (ikizungumzia kanisa la wakati wa kwanza la Efeso, 55,170)

- ✓ Hawa “wadudu wa kirumi” walikula lile tunda – lile runda la roho, ambalo ni upendo wa kiungu, furaha, amani… (Galatia 5:22)
  Je biblia haielezei hilo kimbele.
- ✓ Kwa sababu kuna kuongezeka kwa uasi, upendo wa wengi utapoa. Mathayo 24:12: ufunuo 2:4.
- ✓ Wanaangamia kwa sababu walikataa kuupenda ukweli (Wathesalonike 2:10)

Yule nzige (ikizungumzia kuhusu wakati wa kanisa la Smirna 170 – 312)

- ✓ Alikuja na roho ileile ya kupinga neno na kula yale majani.
- ✓ Ule ushirika wa kiungu, majani yako pale kuleta ubaridi, kwa kivu li wakati wa joto
- ✓ Kwa kukosa huu ufunuo ndiyo maana tunayo migawanyiko mingi kati yetu na dhihaka nyingi, unaona wanakosa ule ufunuo wale walimu! (Hosea 4:6) [5]
- ✓ Sisi sote tunao ufunuo unaokuwa imani yako inaongezeka kwa sababu neno la Mungu linakuwa ule mwili wa Bibi Harusi **(Waefeso 2:20-22; 2Petro 3:18; Matendo 6:7)**

1. Yule Parare (ikizungumzia wakati wa kanisa la Pergamo (312-606)
   - ✓ Alikuja na kula lile gamba (gome)
   - ✓ Kile kifunikio cha kanisa, yale mafundisho ya kiBiblia yaliliwa na kanuni zisizo za kibiblia, maungamo, utaratibu wa mapokeo, viliingizwa – ingawa Yesu alisema katika ufunuo 22:18-19 “Mtu yoyote akiyaongeza, Mungu atamuongezea hay o mapigo hayo yaliyoandaliwa katika kitabu hiki. Na mtu yoyote akiondoa katika maneno ya unabii
   - ✓ Wa kitabu hiki. Na mtu yoyotealiondoa atamuondolea sehemu yake katika mti ule wa uzima……………………ni kule kubadilisha hata neno moja tu kwa kuliandoa au kuliongeza kwake. Ndio hila ya mwanzoni ya shetani katika Bustani ya Edeni. Aliongeza two neno dogo kwa kile Mungu alichosema. Hilo lilimaliza.ilileta kifo na maangamizi.Na katika waefeso, ilikua jambo jambo lilelile. Neno tuu lililo ongezwa, Neno tuu lililo agizwa, na Yule mpinga-Neno,roho ya mpinga kristo ikaanza kustawi. [2]

2. <u>Yule madu madu</u> (ilizungumzia wakati wa kanisa 6060-1520)
   - ✓ Alishambulia mzizi –ule uhai

- ✓ Alishambulia ule utovu-utovu wa uzima
- ✓ Roho Mtakatifu alilazimishwa atulie nje na roho ya kibinaadamu ili aingie ndani mazehebu siyo ya Mungu.kamwe haya kuwa kamwe hayawezi kuwa.Ni roho isiyo sahihi ambayo inawatenganisha watu wa Mungu.kati ya uongozi na washiriki, ni roho isiyo sahihi inayotenganisha watu na watu.hivyo ndivyo madhabahu na vyema vinavyo fanywa, katika kauli kujiundia washiriki wanajitenga wenyewe na neno la Mungu na kujileta wenyewe katika uzinzi wa kiroho. [3]
- ✓ wakati aliondoka Yesu alisema kwamba atamtuma Roho wake ambaye ulimwengu usinge mpokea hiyo ni kweli. Dunia au utaratibu wa dunia haungeweza kumpokea yeye. Hivyo ndivyo mashariki yalivyo- ni taratibu za duniani nionyeshe mimi kanisa lenye utaratibu wa dunia ambalo limejaaRoho Mtakatifu.Nataka kuliona hilo kama ukiweza kunionyesha kanisa la aina hiyo basi umeweza kuona kosa katika neno la mungu. Hapana bwana, hakuna hata moja wa hawa wajumbealiekua katika taratibu za mashariki.Wlitolewa nje au walitoka nje, Itawezekana aje roho mtakatifu awe katika hayo washiriki wakati ni hayo mashariki ambayo yamechukua nafasi ya roho na madhehebu yanachukua nafsi ya neno. Kumbuka mashariki yanachukua nafsi ya neno. Kumbuka mashariki haya Ni"kifo".Haiwezi kuwa vinginevyo. Kama dunia inachukua uongozi Roho mtakatifu anaondoka[6]
- ✓ Walikaa na mawazo yao wenyewe na kwa mashauri yao na kwa namna hiyo waliliweka pembeni neno la Mungu ***(Marko 7:7-9)***

Lakini Mungu ametupa sisi ahadi ya Kiungu ya kurudishiwa/ kurejeshewa.

"Nami nitawarudishia hiyo mamlaka iliyo na nzige, parare na madumadu, na tunutu….

***(Yoeli 2:25-27)*** na kama wajumbe wane wa uzima wamerudisha ule mti .

1. Wa kwanza alikuwa nani? Martin Luther, kuhesabiwa haki kwa imani. Abrahamu alimwamini Mungu. Unaona. Sio kile tulichofanya, Ni kile Mungu alichofanya. Siyo kile ninachoenda kufanya, ni kile alichokwisha kukifanya.
   Ninajua mimi siyo mzuri, sikuwa kamwe na kamwe siwezi kuwa lakini sasa katika uwepo wa Mungu mimi ni mkamilifu hakika.Kwa sababu sio mimi Kamwe haniangalii mimi, Anamuona Kristo. Mimi niko ndani ya Kristo.Na jina langu lilishirikishwa pamoja naye pale katika misingi ya ulimwengu.Nasubiri tuu ile kwamba univute juu.Na tutaenda, katika moja ya siku hizi zilizobarikiwa kwenda kumhani hewani.[7]
   - ✓ Kule kuhesabiwa haki kulirudisha ule utomvu.
2. Ya pili ilikuwa ni nini ? Joni Wesley, ule utakaso.
   - ✓ Utakaso ulirudisha tena lile gamba (gome), mafundisho ya utakaso. [8]
3. Ya tatu ilikuwa ni nini ? Pentekoste. Pamoja na kurudishiwa zile karama, Roho mtakatifu, ubatizo wa Roho Mtakatifu.
   - ✓ Ule mwenendo wa kipentekoste umekuja na Roho Mtakatifu halisi amemwagwa tena (mwanzo 1906 kule lo enjoo).
   - ✓ Uke ubatizo wa Roho Mtakatifu ulitokea na vile vipawa halisi vya kiroho vimerudishwa.

- ✓ Ni kitu gani kilichorudisha yale majani? Wapentekoste. Ni kitu gani? Wapentekoste, majani, wakipiga makofi, furaha, wakifurahia, wapentekoste. [8]

Sasa utaona kwamba kila wakati ulichovya kidogo katika Roho Mtakatifu. Kule kuhesabiwa haki ni kazi ya Roho Mtakatifu. Lakini ule ubatizo ni Roho Mtakatifu,ndiyo sababu ulihitaji kiunabii, nabii aje chini, hakuna mjumbe kwa huwo wakati, kwa sababu Roho Mtakatifu amekuja mwenyewe katika ukamilifu wake wa ubatizo. Lakini mwishoni mwa wakati kama inavyoishia kwa nyinginezo zote, tunaona hapo tena, Yule mjumbe alitumwa, na yale mapungufu yote yanawekwa kila kimoja mahali pake, kama hivyo halafu sasa unyakuo unakuja kwenye kanisa. [9]

Kule chini katika nyakati zote, walipokea Roho Mtakatifu, lakini si kwa kiwango walichonacho leo, kwa sababu ni kurudishwa kule kwa kwanza kama tunavyouchukua ule mshumaa, Alfa na Omega, vile walivyowasha ule mshumaa. Iliendelea kupanda juu na kupnda juu. Na nuru ikapungua na kupungua na halafu ikarudi tena, mwanzo na mwisho na kadhalika.
Lakini katika wakati huu wa kanisa, ule ujumbe unaomwagwandani ya kanisa. Lakini hii maska ni siyo maskani ya Roho mtakatifu. Hakuna kitu kama hicho. Watu binafsi wanaokuja kwenye hili kanisa ndiyo maskani ya Roho mtakatifu (Waefeso 2:19) lakini siyo kanisa katika hilo kundi la mwili. [10]

4. Yanne ilikuwa ni nini? Lile Neno. Nini? Lile Neno.
    - ✓ Ile ya nne ilikuwa Neno, lenyewe, lile neno limefanyika mwili, matunda ya kuthibitisha ishara ya kufufuka hatimaye Kristo baada ya kupandwa kwa utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu, yale mashirika yalikufa, na Kristo kwa mara nyingine tena amejiweka katikati mwenyewe kama kile kifuniko cha piramidi. Mstari wa kwanza kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu halafu baadae kuja kwa kile kifuniko. [8]
    - ✓ Hiyo ni nini? Kule kurudishwa tena kwa siku ya kwanza, kwanza –“naye ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee tena mababa” ***(Malaki 4:5-6)*** kuleta kule kurudishiwa tena kwa ule upetekoste halisi, siyo misisimko ….. na itadhihirisha nuru ya jioni, Jua lilelile ambalo lilionekana wakati wa nuru ya asubuhi, hilo limeahidiwa kwa siku ya leo. Amina. Amina. Tuko wapi marafiki? Tuko wapi? Kule kungoja tuu kuondoka njiani (***2Wathes 2:7-9)*** kadhalika ufunuo 11 linaweza kufahamikakwa wayahudi. Hiyo ni kweli unyakuo unakuja. [11]
    - ✓ Mungu anaunganisha bibi harusi wake, yeye anakuja pamoja, kutoka mashariki na magharibi na kaskazini na kusini. Kuna wakati wa kuunganika na ndio unaoendelea sasa. Anaunganika kwa kusudi gani? Kwa kule kunyakuliwa. Amina! Mungu anamfanya yeye kuwa tayari, ndiyo bwana kuunganika! Kwa nini? Yeye bibi harusi, hiyo ni kweli naye amejiunganisha mwenyewe na bwana arusi, unaona na Yule bwana arusi ni Neno. [12]
    - ✓ Katika ***Yoeli 2:28,*** ameahidi kuwa katika siku hizi za mwisho kutakuwako mvua za vuli zitamwagwa juu ya watu. Amejimwaga yeye mwenyewe.[13] ndani ya kanisa, siyo tu sehemu yake, sio tu kwa umbali ilivyofunuliwa wakati wa Luther, Wesey na Pentekoste, lakini ni yeye mwenyewe kwa ukamilifu wote.
      Huu wakati wasardikia ambao ulianza tuu katika karne hii ya ishirini. Kwanza ni wakati ambao ulitegemewa kwa lile kanisa la kweli litageuka kuwa bibi harusi kama alivyokuwa pale Pentekoste, tunajua ya kuwa lazima kuwe na kurudi zile nguvu za kuendeshea. Waumini walihisi hio katika roho zao na wakaanza

kumlilia Mungu kwa ajili ya kumwagiwa upya kama ilivyokuwa katika karne ya kwanza.

Kile kilichoonekana kama jibu kilikuja kwa wengi kuanza kunena kwa lugha na udhihirisho wa vipawa vya roho. Kwa hiyo iliaminiwa kuwa ni kule kurejeshwa kulikosubiriwa. Hiyo haikuwa hivyo kwa sababu mvua za vuli (baadae) zingekuja baada tuu ya mvua ya kwanza ambayo ni mvua ya kuchipua au mafundisho. Sasa mvua za baadae zina kuwa ni mvua za mavuno. Zinawezaje hizi kuwa halisi wakati mvua za mafundisho hazijaja bado? Yule nabii-mjumbe ambaye angetumwa ili afundishe watu na kugeuza mioyo ya watoto kule kwa mababa wa Pentekoste alikuwa bado hajaja, kwa hiyo kile kilichowaziwa kuwa ni kurejeshwa na nguvu za kuhuisha kwenda kwenye unyakuo zilikuwa bado kuja. Katika huo kulikuwa na mchanganyiko wa wasio haki kupokea Baraka za kiRoho na madhihirisho katikaa Roho Mtakatifu. Kama tulivyokuwa tukiwaambia, katika huwo pia kulikuwa na nguvu za shetani, kwani watu walikuwa chini ya mamlaka ya shetani, na bado inaonekana hakuna waliotambua hilo. Sasa kuthibitisha kuwa haikuwa halisi, hawa watu (hata kabla ya kizazi cha pili hakijatokea) waliunda mashirika, na kuandika mafundisho yao ambayo sio ya kimaandiko na kujenga kuta zao, kama yalivyofanya makundi mengine yaliyowatangulia nyuma.

“Ni hii asema bwana” kwa maana ndivyo ***Yoeli 2:23-26*** alivyosema, “furahi, basi, enyi wana wa sayuni, mkamfurahie bwana, Mungu wenu, kwa kuwa yeye huwapa ninyi mvua za masika kwa kipimo cha haki, naye huwanyeshea mvua, mvua za masika, na mvua ya vuli kama kwanza na sakafu za kupepetea zitajaa ngano. Na mashini kizo yatafurika kwa divai na mafuta. Nami nitawarudishia hiyo miaka iliyoliwa na nzige, na parare na madumadu na tunutu, jeshi langu kubwa nililolituma kati yenu, nanyi mtakula chakula tele na kushiba, na kulihimidi jina la Bwana, Mungu wenu, aliyewatendea mambo ya ajabu. Na watu wangu hawatatahayari kamwe”.

Sasa inasema Mungu ataenda ”kurejesha” wakati wa walutheri haukulirejesha kanisa, ulianza matengenezo, wakati wa Weslwy haukulirejesha, ule wakati wa Pentekoste haukulirejesha, lakini Mungu ni lazima arejeshe kwa maana hawezi kulikana neno lake. Huu sio ufufuo wakanisa Ni “kurejeshwa” Mungu atalichukua kanisa na kulirejesha pale nyuma pentekoste ya mwanzo. sasa angalia mstari wa 25 inaelezea ni kwa nini tunahitaji kurejeshwa. Yule nzige, parare, na madumadu na tunutu, wamekula vyote kasoro mizizi na kisehemu kidogo cha shina. Sasa tunaambiwa kuwa hawa wadudu ni mdudu yuleyule katika hatua tofauti. Hiyo ni sawa na roho ya mpinga kristo ikidhihihirishwa katika mashirika, madhehebu, na mafundisho ya uongo.
Katika nyakati. Na masikini ile mizizi midogo na shina zitaenda kurejeshwa. Mungu haendi kupanda kanisa jipya, lakini anaenda kurejesha ule upanzi wake wa mwanzo kuwa mbegu ile ya asili (mwanzo). Analifanya hilo kama lilivyoelezwa katika mstari wa 23, kwa mafundisho, au mvua za “mwanzo”. Baadaye kutakuja mvua za mavuno au imani ya kunyakuliwa. [1]

Ndiyo Mungu anarejesha neno lake kamili, na tunajua neno la Mungu siyo lisili na nguvu ***(Luka 1:37)*** na tukiwa na kule kurejeshwa kwa neno kutakuja kurejeshwa kwa nguvu. [14]
Kutakuwepo nuru wakati wa jioni ***(Zakaria 14:7)*** Yesu kristo yuleyule jana leo na hata milele. Ule mti wa bibi harusi ulikuja wakati wa Pentekoste, kulikuwa na mti ambao daudi aliona, umepandwa karibu ya vijito vya maji. Mto mmoja (zaburi 1) Yule Roho Mtakatifu, maji yote yakitiririka kuelekea, karama, karama za Rohoni zikitiririka kuuelekea huo na majani yake hayanyauki, utaleta matunda yake. Hiyo ni sawa? Kumbuka utaleta matunda yake kwa majira yake. Ule mti mkamilifu kristo, ulikuja.Na alipokuja kulitokea nini? Walimkatilia yeye chini, wakamtundika kwenye mti wa kirumi. Lakini alifufuka tena. Hiyo ni kweli yuko hapa leo. [15]

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Luther<br>1483 – 1517 | | Wesley<br>1703 – 1791 | | Pentekoste<br>Kutoka 1901 | | Kuunganisha wakati<br>Wakati wa kurejesha kikamilifu. |
| Maazimio 95 ya Luther | | Whitefield<br>(1714 – 1770) | | R.A.T orrey<br>(1856 – 1928) | | Mahali 4:5-6<br>Daniel 12:4,9<br>Ufunuo 10:7<br>Luka 17:30<br>Waefeso 1:15-17 |
| | | C.G Finney<br>(1792 - 1878 | | Charles Alexander<br>(1902) | | |
| Philipp Melanchthon<br>(1497 – 1560) | | Charles Spurgeon<br>(1834 – 1892) | | Evan Roberts in Wales (1905) | | Yale maisha halisi ya Yesu Kristo yamekuja tena. Yeye mwenyewe, sio kazi ya Roho Mtakatifu, ila ni Roho mtakatifu kwa utimilifu wake wote anakuja. |
| Huldreich Zwingli<br>1484 – 1531 | | Dwight Moody<br>(1837 – 1899) | | Azusa street mission pastor Barret. William Seymour (1906) | | Ule utu wa Roho Mtakatifu umekuja katika siku za nao utakuwa pamoja nasi, na kuwa ndani yetu. |
| Johannes Calvin<br>(1509 - 1564)<br>Na watengenezaji wengine<br>John Smith (1609) Baptist<br>Kuhesabiwa haki: Kipawa cha Mungu mwenye haki ataishi kwa imani (Rum. 1:17) | | Hadson Taylor<br>(1832 – 1905)<br><br>Utakaso na ukamilifu wa mkristo yalikuwa mambo 2 aliyoshughulika sana nayo John Wesley | | Uamsho wa kipentekoste kurudishiwa kwa vipawa, neema na nguvu za kimiujiza. | | Ule ukamilifu wa neno umekuja na kudhihirishwa au kule kufunguliwa kwa mihuri saba ambayo imeahidiwa kwetu katika wakati huu.Yule mwana wa Adamu amerudi tena kanisani alifunuliwa ndani ya wanadamu.Yeye,Bwana harusi anajiunganisha mwenyewe na bibi arusi wake. |

***Ni kazi za Roho Mtakatifu au sehemu (kwa kipimo) ya Roho Mtakatifu, lakini sio kwa ukamilifu wote wa Roho Mtakatifu mwenyewe.***

Yeye ni mti ule wa bwana Harusi. Hapo sasa mti ule wa bwana harusi, bila mti wa kike (mama) hauwezi kuzaa matunda, kwa hiyo ni lazima apate mti wa bibi harusi. Ni lazima huo mti mama uwe kwa jinsi hiyo hiyo. Lile neno lilifanyika mwili ndani ya ule mti. Lazima iwe ni uhai uleule katika mti huu wa kike (mama) kama ilivyo kwa bibi harusi. [8]

Sasa ile nuru ya wakati wa jioni inaangaza katika ile mbegu ambayo imekusudiwa kimbele, na wale waisraeli wa kiRoho walio miongoni mwa wayahudi na mataifa watahuishwa (Ezekiel 37:1-10)

Bwana analeta hatua nne za kurejeshewa juu ya ile mifupa (mikavu) iliyokuja. [8]

1. Nami nitatia mishipa ndani yenu.
    - Luther – sio kwa matendo bali ni kuhesabiwa haki kwa imani
2. Nami nitatia nyama iwe juu yenu.
    - Wesley – Kutakaswa/ kusafishwa na kuandaliwa kwa huduma ya Mungu.
3. Nami nitawafunika ngozi juu yenu.
    - Ubatizo wa Roho Mtakatifu na kurudishiwa kwa vipawa vya Kiroho.
4. Nami nitaleta pumzi ndani yenu nanyi mtaishi.
    - Yeye Roho Mtakatifu wmenyewe anakuja katika Kanisa lake.
    - Yule mwana wa Adamu – Kristo, lile neno lenyewe (Luka 17:30) – amejifunua mwenyewe. [8]

- ➢ Maana ya Luther ilikuwa ni ujumbe na udhihirisho wa kuhesabiwa haki.
- ➢ Ujumbe wa Wesley ilikuwa udhihirisho wa kutakaswa.
- ➢ Pentekoste ilikuwa kurejeshwa kwa vipawa.
- ➢ Lakini huu ni kulitambulisha lile jiwe la kifuniko, siku ya mwisho, ule mti wa bibi arusi, ambayo ni tofauti na vyote hivyo. [16]

**Nukuu za Kiingereza**

[1] Kitabu cha nyakati saba za Kanisa UK. 366,377 – 379.

[2] Wakati wa kanisa wa efeso CAB uk. 92.

[3] Wakati wa kanisa la Pergamo CAB uk. 197, 206.

[4] Nitawarejeshea (57 – 0309B) Aya E-12

[5] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa (63 – 0728), Aya 304

[6] Wakati wa kanisa wa Sardi.

[7] Ile sheria ilikuwa ni kivuli (56 - 0621), Aya E – 47

[8] Kurejeshewa kwa mti wa bibi arusi (62 – 0422) Aya 230, 415, 505, 510.

[9] Maswali na majibu juu ya mihuri (63 – 0324 M), uk.464

[10] Majina ya makufuru (62 – 1104M) Aya 121 – 123

[11] Makao ya baadae (64 – 08021) uk. 62 – 63

[12] Ile ishara ya kuunganika kwa wakati (63 – 0818), Aya 91.

[13] Mungu mkuu aliyefunuliwa mbele yetu (64 – 0629) Aya 91.

[14] Wakati wa kanisa wa laodikia CAB UK. 363

[15] Kuvaa silaha zote za Mungu (62 – 0607) Aya E – 102.

[16] Kuna mtu hapa anayeweza kuwasha taa 63 – 1229M) Aya 162.

Jiwe la kiroho la kujengea na. 43 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*